

Je Kanisa la Sayuni (au Shincheonji) ni la kweli?

Kanisa la Kristo la Shincheonji (*Shincheonji Church of Jesus kwa kifupi (SCJ)*). Ni Imani iliyoanza nchini Korea Kusini na ilianzishwa na mtu ajulikanaye kama **Lee-Man-Hee**

Shincheonji ni lugha ya kikorea yenye maana ya “**Mbingu mpya na Nchi Mpya**” ...Imani ya Shincheonji inafundisha kuwa muasisi wa Imani hiyo yaani Lee-Man-Hee ndiye Mchungaji aliyeahidiwa wa Agano jipya, na yeye pekee ndiye mwenye uwezo wa kukielewa kitabu cha Ufunuo na kukifunua mafumbo yake.

Lee-Man-Hee anafundisha kuwa mtu yeyote ambaye hatakuwa katika Imani yake basi siku ya mwisho hatapokea msamaha, bali atahukumiwa milele.

Imani ya Shincheonji inafundisha pia kuwa... Majina ya makabila kumi na mawili ya wana wa Israeli yamechukuliwa kutoka kwa majina ya wanafunzi kumi na wawili wa Yesu, na inafundisha pia ile idadi ya walioitiwa muhuri katika *Ufunuo 7:4 (wale 144,000)* ni washirika wa *makabila 12* ya Shincheonji jambo ambalo si kweli, kwani biblia

imesema wazi kuwa ni *makabila* 12 na tena imetaja majina yake.

Lakini pia Imani ya Shincheonji inafundisha kuwa Malaika wote ni wanadamu, jambo ambalo pia si kweli kwani biblia imeweka wazi kuwa kuna Malaika na pia wapo wanadamu, **1Wakorintho 4:9,** **1Wakorintho 13:1 na Ufunuo 9:15** inaelezea Zaidi

Imani ya Shincheonji inazidi kufundisha kuwa *Ufunuo* 7:2 inaelezea Taifa la Korea (*Mashariki*) na Lee-Man-Hee ndiye malaika yule wa kwanza, Zaidi sana inamtaja Lee-Man-Hee kwamba ndiye Yohana mpya ambaye amechukuliwa juu mbinguni na kuonyeshwa yaliyopo kule sawasawa na **Ufunuo 4:1**, Imani ya namna hii pia ilizuka kwa baadhi ya watu nchini Nigeria akiwemo **Amos Segun** na baadhi ya watu Ulaya katika karne ya 20 mwanzoni na 21 mwishoni, wakidai kuwa wao ni Yohana, kama anavyodai sasa Lee-Man-Hee, na Imani zao zikakomba idadi kubwa ya watu lakini wote hawakufanikiwa katika uongo huo.

Sayuni Christian Mission Center ni mkono wa elimu wa Kanisa la Shincheonji ambao Juhudi zake za kimsingi za imani ya chuo hicho ni kuwaalika watu kuhudhuria madarasa katika vituo vyao mbalimbali,.

Na Wasomaji wanapohitimu, wanasemekana kuwa “wametiwa muhuri” kama washiriki wa 144,000, na hivyo mwisho wa siku wataokolewa,

jambo ambalo si kweli kibiblia kwani idadi ya 144, 000 biblia imeweka wazi kuwa ni wayahudi ambao watatiwa Muhuri wakati wa kipindi cha dhiki kuu, wakati ambapo injili itarudi Israeli.

Chuo cha Sayuni Christian Mission Center inatoa viwango vitatu vya masomo ya kozi.

Katika kozi ya ngazi ya mwanzo (*Maarifa ya Kweli ya Siri za Ufalme wa Mbinguni*)

wanafunzi wanafundishwa **“maana ya kweli ya mifano iliyοandikwa katika Biblia.”** Ikiwa wanafunzi hawaelewi mafumbo kwa usahihi, anadai Lee Man-hee, **“hawawezi kusamehewa wala hawataokolewa.”**

Kozi ya ngazi ya pili inatoa muhtasari wa Biblia ambao, kulingana na Lee Man-hee, utasaidia wanafunzi “kufahamu muktadha wa jumla wa Biblia” ili kuwasaidia katika kujifunza na wokovu wao wa mwisho.

Ngazi ya tatu na ya mwisho inashughulikia Kitabu kizima cha Ufunuo.

Kufikia mapema Agosti 2024, kulingana na Shincheonji, makanisa **1,352 katika nchi 41** yamebadilisha ishara zao na Imani zao na kuzifuata zile

za Kanisa la Shincheonji Church of Jesus na Zaidi wanatuma maombi ya kuomba kutumiwa wakufunzi na elimu hiyo.

Zaidi walengwa wa kwanza wa elimu ya Shincheonji ni wachungaji wenye makanisa tayari, kwani wanaamini kwa njia hiyo itakuwa rahisi kuifikisha Imani mbali Zaidi.

Shincheonji amekuwa akitumia "kutabiri" kama njia za uinjilisti kwa baadhi ya makundi. Wanawakaribia vijana na wataalamu kupitia shughuli za klabu zilizojificha, uwekaji kazi, na tathmini za kisaikolojia. Kwa wazee, hutoa bahati nasibu bila malipo mitaani ili kukusanya habari za kibinafsi. Mbinu zao zinahusisha namna mbalimbali za kujificha na kudanganya, wakijihuisha katika utendaji unaonyonya dini ili kufuata masilahi ya kikundi.

Zaidi ya hayo yapo mambo mengine ndani ya Shincheonji yaliyo kinyume na biblia, lakini kwa hayo machache itoshe kusema kuwa Imani hii, si ya KRISTO YESU, imebeba upotoshaji ambao unao msingi wa mafundisho ya Uongo, na pia msingi wake ni IMANI katika MTU, Zaidi ya katika KRISTO YESU.

Bwana akubariki.

Maran atha.

Shalom.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

ORODHA YA IMANI POTOFU- Sehemu ya 1.

IMANI “MAMA” NI IPI?

Fahamu Namna ya Kuomba.

IMANI YENYE MATENDO;

Je maombi ya mlimani yana ulazima wowote kwa mkristo?

**MAMBO (2) YATAKAYOKUTENGA NA IMANI SIKU HIZI ZA
MWISHO.**

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp

Print this post